KUJIANDAA KWA AJILI YA UINJILISTI

1. Maandalizi ya binafsi kiroho ni muhimu kuliko vyote

Katika Yohana sura 4, Yesu anazungumza na mwanamke kisimani. Zilikuwepo sababunyingi sana ambazo zingefanya Yesukuzungumza na yeye mwanamke.
- Alikuwa amechoka, hali ilikuwa ya joto, kuu na njaa. (4:6).
- Kiutamaduni wanaume na wanawake hawakuruhusiwa kuzungumza kwenye hadhara.
- Wayaudi na Wasamaria hawakuchangamana (4:9).
- Yesu alijua kwamba yule mama alikuwa na sifa mbaya alikubali kuhatarisha heshima yake (4:17).

Hata hivyo Yesu alizungumza naye. Alikuwana utayari na umkini kiroho kiasi cha kuionakila fursa iliyokuwa mbele yake bila kujali kikwazo.

Kujiandaa kwako kiroho ni kwa muhimu sana katika kushuhudia muumini anahitaji njia kadhaa za maandalizi.

. Kuombea fursa
. Kutafuata fursa
. Kuvikwa nguvu ya kuitendea kazi fursa

Kama ilivyoelezwa mwanzoni kama umejiandaa kiroho na uko makini mara nyingi utajikuta katika mazungumzo ya kiroho.

Maana ya Ukristo hukupa zana rahisi za kukuwezesha kutawala fursa hizo. Jambo lile la kwanza na la pili ni swala tu la nidhamu ya binafsi ya kiroho. Kama hujiandai na kutafuta fursa kwa hakika fursa hizo zitakupita.

2. Kutumia fursa katika mazingira ya kawaida

Mara kwa mara wakristo hupata nafasi za kuweza kuzungumza na marafiki zao kuhusu mambo ya kiroho. Lakini nafasi hizo maranyingi hupotea bila ya injili kuhubiriwa.

Hebu ona hapa jinsi Yesu alivyoitumia nafasi aliyoipata ya mazungumzo na mwanamke Msamaria.
- Mazungumzo yalianzia kwenye maji ya kawaida. (4:7)na kumpa nafasi Yesu kuzungumzia' maji ya uzima(ya kiroho)' (4:10)
- Kupokea kwa mwanamke kunatoa Nafasi kwa watu wa mji wa Sikari. 'Njooni mwone…', anasema (4:29)
- Huduma yake kwa watu wa mji inatoa nafasi kwake kukaa siku mbili ambazo hakuwa amepanga (4:40). Hivyo mazungumzo yale ya awali ya kwanza yakafanyika kuwa kipindi kizuri cha muda wa mafundisho yakuendelea.

Kama ilivyoelezwa mwanzoni kama umejiandaa vema kiroho na uko makini mara nyingi utajikuta uko katika mazungumzo ya kiroho.

Maana ya Ukristo hukupa wewe mwongozo ulio rahisi wa kukuwezesha kuzitumia fursa zinapotokea.

Kumbuka katika kushuhudia mtu kwa mtu *maandalizi ya binafsi ya kiroh o ni muhimu kuliko vyote.*

2

Injili rahisi sio rahisi kueleweka

Ni kwa nini watu wengine hawawezi kuelewa hata ile injili iletwayo kwa lugha rahisi kabisa Hebu tuone sababu.

Siku za karibuni kundi la wakristo liliulizwa kama ungeambiwa uandike maelezo rahisi kabisa ya injili kikristo ni dhana ipi ya kibiblia au theolojia ungeichagua?

Majibu yalikuwa kama ifuatavyo
1. Tabia ya Mungu (muumbaji, upendo)
2. Dhambi
3. Mungu alimtuma Yesu
4. Mauti yake kwa ajili ya dhambi zetu
5. Ufufuo
6. Toba
7. Imani

8. Wokovu kwa neema Injili rahisi “kwa kawaida itakuwa na mengi yahusuyo dhana hizi. Lakini kumbuka wengi leo hawauelewi ujumbe wa ukristo. Hivyo kwa mazungumzo ya mara moja kwa haraka tunajaribu kutoa maelezo kwa kutumia dhana nane kwa mtu kusikiliza, kuelewa na kutafakari na tunatarajia aitikie kwa wakati mmoja.

Ni sawa na kuchukua mlo wa kula kwa hatua nane na kuuweka wote katika sahani moja na kumpa mtu na kumwambia ale wote. Baada ya dhana ya kwanza au ya pili watu hupata hali ya kuvimbia kiroho na kuanza kutoa matamko yenye ufahamu finyu kwa hakika hawaelewi kinachosemwa.

KWA AJILI YA MAJADILIANO

Soma Yohana 4:31-42

1. Mistari 31-34.

Ni chakula gani ambacho Yesu anasema atakula katika kifungu hiki

2. Mistari 35 – 38

je watambua kuwa kuna mavuno yaliyotayari katika eneo lako? Ni kitu gani kifanywe?

3. Mistari 39-42

kwa nini Yesu aliendelea kukaa siku mbili na wasamaria nje ya ratiba yake?

Je hili lahusiana na dhana ya kwenda hatua kwa hatua?

4. *Linganisha mistari 19,29,na 42*

Je tathmini ya kuhusu Yesu ilkuwaje ?

Kujifunza kufundisha injili

Ni muhimu kujua kwamba twahitaji kuondokana na dhana kwamba twaweza kuipeleka injili kwa urahisi kwa mara moja kimsingi kuna maeneo itakuwa hivyo lakini kwa ujumla hali hiyo inaendelea kupungua nguvu twahitaji kujifunza kufundisha injili na kuweza kutoa muda wa kutafakari dondoo za
mada hiyo.

Maana ya Ukristo kina lengo la kutoa zana moja ya kufundisha injili kwa kipindi cha muda mrefu

Uinjilisti katika agano jipya

Uinjilisti katika agano jipya ulikuwa wa kuzingatia hali na mahali. Hivyo namna ya kufikia watu na wakati mwingine hata ujumbe uliotolewa kwa jinsi tofauti kutegemea na mazingira. Matokeo yake ni kama tunavyoona katika mfano wa mlinzi wa gereza kule Filipi (Matendo 16:25 – 35)

Hata hivyo ushahidi kwa ujumla kututaka kuendelee mtazamo wa ufafanuzi wa injili zaidi. Mfano:-

kwa Sabato Paulo alijadili nao kutoka katika
maandiko alielezea na kuthibitisha ya kuwa
kristo ilibidi afufuke kutoka kwa wafu baadhi
ya wayahudi walishawishika
Matendo 17:2-4

Hivyo maneno haya hujaribu kuelezea mfumo wa uinjilisti wa agano jipya kiujumla *majadiliano, ufafanuzi, uthibitishi, ushawishi,*
kwa ujumla mitume na wainjilisti hawaonekani kwamba walihubiri injili kwa mtindo mmoja na kutarajia matunda ya haraka. Na inaonyesha pia kwamba wakati mwingine hata hawakuuliza watu maamuzi yao. Wale walioguswa ndio waliwauliza wahubiri.

***Maana ya Ukristo* ni nini ?**

Maana ya Ukristo ni upelekaji wa injili wenye vipengele sita ambao una lengo la kufundisha misingi ya imani ya kikristo. Kozi hii inalenga maandiko ya kitabu cha injili ya Marko kwa kuwa kina maelezo yaliyo rahisi zaidi. Tunachukulia kwamba yule anayepelekewa injili hajui chochote kuhusu Yesu na Biblia.

Ni kozi ya kiinjilisti ambayo ina lengo la kumfikisha mtu kwenye toba na imani halisi afikapo mwisho wa hatua ya sita.

Ni mtindo ambao haumshurutishi mtu kufanyamaamuzi ingawa mara kwa mara kwa ufasaha ataonyeshwa hitaji la kufanya hivyo kozi ikiwa ya endelea.

Kila kifungu katika mfululizo wa kozi hukusaidia kufundisha dhana moja tu, hii humaanisha kulenga jambo moja tu kwa somo. Kila kipengele ni cha kiuinjilist na

hivyo kila mwisho wa kipengele kimoja kuna wito wa kumwamini Yesu.
Katika masomo matatu ya kwanza kazi humjengea msikilizaji ufahamu wa habari za Yesu Kristo na kazi aliyomaliza ya kuwa yeye ni mwna wa Mungu, kifo chake kwa ajili ya dhambi zetu, na ufufuo wake.
Wakati masomo haya matatu yakiendelea, mlengwa hutiwa moyo kusoma injili ya Marko.
(uzoefu huonyesha kuwa watu wazama wengi hufanya agizo hilo)
Katika masomo matatu yaliyobaki tunalikabili swali.
Kazi ya Yesu iliyomalizika inanihusuje mimi?
Narudia tena kila somo litalenga na kufafanua fundisho moja tu.
4
Kazi inaendelea na wazo kwamba baadhi ya watu katika kundi lako hawajui chochote kuhusu imani ya kikristo.
Wengine hawatajua namna ya kupata vitabu vya biblia au hata tofauti kati ya Agano la kale na Agano jipya.
Tunadai kwamba tutauelezea ukristo kwa hatua sita za saa moja moja. Hilo ni dai kubwa kwa hakika kozi yetu ni lazima iwe rahisi na iliyochambuliwa kwa makini.
Hatukusudii kuchanganya fahamu zao kwa kozi kamili ya theolojia ya biblia.
Kozi imegawanyika katika nusu mbili za masomo matatu matatu.

• **somo 1, 2, na 3**
maisha, mafundisho na madai ya Yesu
(kutoka katika kitabu cha Injili ya Marko)

• **somo 4, 5 na 6**
hii inanihusuje mimi

(1) YESU MWANA WA MUNGU
(Kazi ya nyumbani soma Marko 1-5)
(2) YESU: KUSULUBIWA KWAKE
(Kazi ya nyumbani soma Marko 6 – 10)
(3) YESU: UFUFUO WAKE
(Kazi ya nyumbani soma Marko 11-16)
(1) WOKOVU: NEEMA SI KAZI ZETU
(Kazi ya nyumbani soma kipeperushi)
(2) WOKOVU: MKRISTO NI NANI?
(i) toba
(3) WOKOVU: MKRISTO NI NANI?
(ii) Imani
Tumetumia Injili ya Marko kwa sababu
- Ni fupi kuliko zote
- MsamIati wake ni rahisi zaidi
- Sura za kwanza hazina maelezo ya vizazi kama katika Mathayo 1 na Luka 1 – 3, na katika Yohana! Kuna dhana ngumu ya “neno”!

Dondoo muhimu katika kuiongoza kozi

1. Kufungua
Kabla ya kuanza somo ni muhimu walengwa kuwa katika hali ya utulivu pasipo hofu yoyote.
Kama tulivyoona huko nyuma watu hukabiliwa na hofu kuu tatu
• Kwamba wataulizwa maswali na kutokujua kwao kutawaaibisha
• Kwamba watatakiwa kuomba
• Kwamba watatakiwa kusoma kwa sauti
Maneno yako ya ufunguzi yatumike kuondoa hofu hizi.

2. Wakristo (waaminifu) wawe nje ya kundi.
Kama unafundisha kundi jaribu kuwaweka waamini nje ya kundi kadri iwezekanavyo isipokuwa wale ambao tayari ni washiriki kama tulivyosema mwanzoni baadhi ya wakristo hawawezi kujibu maswali yale ya msingi kwa mtindo huo wale wageni wataji ficha kabisa.

3. Ukaaji
Kaeni kwa namna ya duara na mwalimu akae pale atakapoonekana kwa urahisi.
Mwanafunzi akae katika hali ya kawaida akimsikiliza mnenaji ambaye atakuwa ni mwalimu

UTANGULIZI WA MASOMO SITA

MASOM O SITA

5

4. Kazi ya mwalimu
tunajaribu kutoa maarifa (elimu) kuhusu.
5. Muda kwa kila hatua
Tumia dakika 60 – dakika 75 kwa kila hatua kila somo litachukua dakika 30 kufundisha kama kungekiwa hakuna majadiliano lakini majadiliano ni lazima yawepo na yachukue nusu ya muda utakaotumika.
6. Jihadhari na maswali yanayokutoa nje ya somo
Kila swali na mjadala vitiliwe maanani na jaribu kutoa majibu fasaha. Lakini jihadhari na maswali yanayoweza kutawala mjadala na kukutoa katika somo halisi. Kama swali au wazo ni la muhimu basi laweza kujadiliwa baadae wakati wa kunywa kahawa au liachwe kwa kipindi kingine ili liweze jadiliwa kwa kina zaidi
7. Vifungu vya Biblia
Vinapotajwa vifungu vya Biblia vifunguliwe na kundi na kusomwa unapotaja kifungu taja na ukurasa wa biblia pia.

Kusudi

Kusudi la somo hili ni kuwatambulisha watu kwa Yesu hasa huduma yake ya awali.
Tumeitazama miujiza yake na mamlaka yake ikimdhihirisha kama mwana wa Mungu

SOMO LA KWANZA

YESU – MWANA WA MUNGU

6

Mwanzoni

• Utahitaji Agano jipya yakawaida tumia tafsiri inayoeleweka vizuri
• Fanya utangulizi wa kuchangamsha ukimkaribisha kila mtu.
• Eleza ingawa kozi imeandaliwa na kanisa x haina lengo lolote kidhehebu. Bali utapitia maeneo yake ambayo yanamakubaliano ya pamoja kati ya makanisa.
• Wahakikishie kwamba hawataulizwa kuomba, kusoma biblia kwa sauti au kujibu maswali hata hivyo utakuwepo muda wa kutosha kujadiliana.
• Watiemoyo kufanya kozi yote kwa wiki sita hadi mwisho.
• Uliza kama kuna wazo lolote kuhusu jinsi kikundi kinavyopaswa kuendeshwa.

SEHEMU YA KWANZA

1. Matamko manne ya ufunguzi

• Kichwa cha kozi hii ni maana halisi ya ukristo
• Ukristo kama jina lilivyo unamhusu Yesu Kristo tu
• Kumbukumbu pekee tulizonazo kumhusu Yesu ni yale yaliyoandikwa kuhusu maisha yake katika injili nne – Mathayo, Marko, Luka na Yohana.
• Katika wiki chache zijazo tutaangalia moja kati ya hizo, injili ya Marko. (wape Agano jipya na lisaidie kundi kufungua kitabu cha Marko)

2 Soma, chambua

Anza kwa kufungua Marko 1:1 “Mwanzo wa injili ya Yesu Kristo, mwana wa Mungu” inamaanisha nini kusema Yesu ni mwana wa Mungu? Tutaona leo kwamba Yesu ni mtu wa madaraka - mamlaka yote ya Baba yake. Kwa mfuatano, kufungua vifungu hivi vifuatavyo kisha toa maelezo mafupi kwa kila kimoja.
(a) MARKO 1;21, 22 MAMLAKA YA YESU KAMA MWALIMU
Watu walishangazwa kwa jinsi vile Yesu alivyofundisha. Hakuhukumu mawazo ya Rabi au walimu wengine alifundisha kwa kusema, “mimi awaambia……”
(b) MARKO 1;23 – 28 MAMLAKA YA YESU DIHIDI WA PEPO WABAY
Akiwaponya wenye pepo kwa neno lake

(c) MARKO 1;29–31; 2:1-12 MAMLAKA YA YESU DIHIDI WA MAGONJWA

Kwa neno lake mtu huyu aliponywa Biblia imenakili matukio ya aina hii zaidi ya 30 – wagonjwa, vipofu, viwete, wenye ukoma wote waliponywa. Uliza kundi kama lina ujuzi wowote wa uponyaji wa jinsi hii. – swali hili laweza kuwa mwanzo wa changamoto.

(d) MARKO 2:1-12 MAMLAKA YA YESU KUSAMEHE DHAMBI

Yesu akamwambia yule mtu "umesamehewa dhambi zako" wakuu wa dini waliliona hili moja kwa moja kama ni dai la kuwa sawa na Mungu Agano jipya yote yatuambia kuwa Yesu yu sawa na Mungu akiwa mwana wa Mungu – zaidi ya hayo yu Mungu na mwanadamu katika nafsi moja (tilia mkazo hapa).

Hivyo hii ndiyo picha tunayoijenga. Yesu amekuja katika uumbaji wa Mungu, dunia ya Mungu akiwa na mamlaka yote ya Mungu.

Hakuna sehemu yoyote ya uumbaji – wanyama, miti, wanadamu na hata ulimwengu wa roho – ambao hauko chini ya utawala wa Yesu. Akiwa Mungu katika umbile la mwanadamu aliweza kusamehe dhambi.

Hata hivyo kuna eneo moja la mamlaka ya Yesu twahitaji kuliona.

(e) MARKO 4:35-41 MAMLAKA YA YESU JUU YA SILI

akiweza kutuliza upepo mkali wa dhoruba na bahari ikawa shwari.

(f) MARKO 5:35-42 MAMLAKA YA YESU JUU YA USIMA NA MAUTI

Katika sehemu tatu tofauti alifufua wafu – hata Lazaro alikaa kaburini siku nne.

(g) MARKO 1:16-20 MAMLAKA YA YESU JUU YA WATU

Yesu aliwaendea watu ambao walikuwa wageni kabisa kwake na aliwaamuru kuacha ajira zao na familia zao wamfuate. Akiwa mwana wa Mungu Yesu hutuita vile vile wewe na mini watu wa kawaida tumfuate.

Hawa watu wanne walimfuata. Baadhi yao aliowaita badaye hawakumfuata. Katika uumbaji wote mamlaka ya Yesu haiwezi kupingwa isipokuwa tu kwa utashi wa watu.

Hata hivyo Mungu hutuamuru tunyenyekee chini ya mamlaka ya mwanawe. (sisitiza kuwa hatuagizi kuwa waache familia zao au wenzi wao).

(3) Tamati

Tumeona katika somo hili

a) Anayo mamlaka kuu akiwa mwana wa Mungu na ni Bwana mkuu katika uumbaji wa Mungu

b} Dai lake la kuwa na uweza wa kiungu

c) Haja ya kufanya uamuzi kumhusu yeye. Mtummoja alisema Yesu ni mtu ambaye haiwezekani kumdharau waweza kumkataa na kumwita mwongo mwenda wazimu au waweza kumtumikia kama Bwana.

Ingiza wazo la kiti cha miguu mitatu (stuli) –

Dhana tatu kuu ambazo ndizo kiini cha imani ya ujumbe wa kikristo.

4. Kazi ya nyumbani

Liagize kundi kusoma Marko hadi 5 waweza kutoa nakala ya mpango wa kusoma ulioko mwisho wa kitabu hiki yabidi waweke alama mahali wasipoelewa au pale watakapotaka kufanya majadiliano muda utakaotolewa kwa kipindi cha wiki ijayo kujadili maswali yao na yale waliyopokea mwanzoni mwa somo la wiki ijayo. Wape kitini (handout) namba 1

KADI ZA KUFUNDISHA

Tandaza hizi juu ya sakafu au meza

MAMLAKA YA YESU

1…..KAMA MWALIMU

2….. MAMLAKA YA YESU DIHIDI WA PEPO

3…. MAMLAKA YA YESU DIHIDI WA MAGONJWA

4... **….**MAMLAKA YA YESU KUSAMEHE

5 ……MAMLAKA YA YESU JUU YA SILI

6. ……MAMLAKA YA YESU JUU YA USIMA NA MAUTI

… ..MAMLAKA YA YESU
JUU YA WATU
(wewe na mimi)
9

Dhumuni

Dhumuni la somo hili ni kujenga kutoka katika somo la lililopita ya kwamba Yesu hakuja tu kuwa mponyaji mkuu na mwalimu kufa na kufufuka kwake ni matukio ya muhimu sana katika Imani ya Kikristo.

SOMO LA PILI

1. Kkupitia kazi ya nyumbani

Wanakikundi watakuwa wamesha soma Marko 1-5 waulize kama wanayo maswali yatokanayo na sura walizosoma kuhusiana na imani ya kikristo. Toa muda wa majadiliano ambao. Endapo maswali yatakuwa mengi yaandike na yale utakayoweza kuyajibu wakati huu yajibu na mengine waweza kuyajibu vizuri zaidi baadaye.

2. Marudio ya somo la kwanza

fanya marudio ya dakika mbili ya somola kwanza, “YESU – MWANA WA MUNGU”
kurudisha kumbukumbu za wanafunzi.

3. Kkweli za msalaba

Soma Marko 15:3-38

Wajulishe kuwa msalaba ni kiini cha imani ya kikristo. Msalaba umekuwa ni alama ya kanisa. Lakini ni nini hasa kilitokea katika yale masaa sita Yesu alipokuwa msalabani.

(a) Giza (15:33)

Giza hili la Kiungu liliashiria kuwa tukio la kiungu lilikuwa likitokea wakati haikuwa nikupatwa kwa jua kama ilivyokuwa wakati wa mwezi mpevu wakati wa pasaka.

(b) Kilio (15:34-37)

Watu wengine hufikiri kuwa kilio hiki” kwa nini umeniacha?” huonesha upungufu wa imani wa Yesu kwa Mungu Baba. Lakini lazima tuuone ukweli wa kilio hiki kwamba hakika Mungu kwa kiasi Fulani alimwacha Yesu msalabani.

Ielezee ile dhana ya Yesu kuteswa kwa niaba yetu ukitumia ufafanuzi wa kitabu (tazama ukurasa 46) Eleza kwamba Yesu alichukua hatia yetu na adhabu yetu (hii yamaanisha ghadhabu ya Mungu) yote mwilini mwake pale msalabani. Pia ongezea kwa kuelezea ya kwamba ufufuo ulidhihirisha kuridhishwa kwake Mungu kwa ile kazi aliyoifanya Yesu pale msalabani.

(c) Pazia (15:38-39)

Toa maelezo mafupi kuhusu muundo wa hekalu, lilikuwa na chumba kidogo na kikubwa. Chumba kidogo husimama badala ya makao ya Mungu na chumba kikubwa makao ya makuhani. Jielezee dhana ya upatanisho kupitia kupasuka kwa pazia.

Habari njema ni kwamba urafiki wa Mungu na wanadamu umerejeshwa upya.

(d) Hitimisho (10:45)

Wajulishe kwamba kifo cha Yesu kinatosha kabisa kwa dhambi za yeyote. Hata hivyo msamaha wa Mungu hautolewi moja kwa moja kwa kila mtu. Kama mtu hakubaliani na kile lichofanya Yesu msalabani yeye atakuwa anamwambia Mungu kwamba, “Sihitaji kubebewa dhambi zangu na yeyote – ntazibeba mwenyewe” na hivyo atazibeba siku ya mwisho. Twapaswa kibinafsi kwa imani kumkubali Yesu wa msalaba.

SOMO LA PILI

YESU – KUSULUBIWA KWAKE

10

4. Hitimisho

Eleza dhahiri kwamba kifo cha yesu kinatosheleza dhambi za kila mtu.

Hata hivyo, msamaha wa Mungu haujiingizi wenyewe kwa kila mtu. Kama mtu hakubali alichofanya Yesu, kimsingi anamwambia Mungu, "Sihitaji mtu yeyote kunibebea dhambi zangu- nitazibeba mwenyewe." Na kwa hakika watazibeba , ile siku ya mwisho.

Tunalazimika kumpokea Yesu wa Msalaba kwa imani.

5. Ufafanuzi wa kiti

Eleza dhahiri kwamba kwa sasa tumeona dhana mbili za msingi za kiini cha ukristo.

6. Kazi ya nyumbani (homework)

Liagize kundi kusoma marko 6-10 nyumbani waweke alama vifungu wasivyovielewa au vile wanavyotaka kuvijadili muda utatolewa kwa ajili ya majadiliano mwanzo wa kipindi cha wiki ijayo Wape kitini cha somo la pili

11

Kitabu

Hiki ni kielelezo kinachofaa kutumika katika somo la pili dhumuni la kielelezo hiki ni kuonyesha maana ya kusulubiwa hasa kwa niaba ya wengine

Utahitaji kitabu kikubwa kinene, usitumie biblia. Liambie kundi kuwa historia ya mmoja Utahitaji kitabu kikubwa; usitumie biblia.

Liambie kundi kuwa kitabu kile husimama badala ya historia ya mmoja wenu katika kundi kuanzia anazaliwa (ukurasa1) mpaka siku ya kifo chake (ukurasa wa mwisho)

Ndani ya kitabu yameandikwa yote tuliyotenda kila tulipovunja amri ya Mungu – kila tendo ov u, kila neno baya, na kila wazo baya kwa mfano Yesu anasema kumchukulia mtu mwingine ni sawa na kuua kwa mtazamo wa Mungu kumtamani mtu mwingine ni sawa na kufanya uzinzi moyoni mwako.

Liambie kundi kwamba ziko kurasa nyingi nyeusi ndani ya vitabu vyao ambazo ungependa wazisome, na kama wao ni waaminifu watadhihirisha ukweli huo.

Nyoosha mkono wako wa kushoto ukielekeza kiganja juu, na kusema. Kwa mfano huu mkono ni wewe na dari linasimama badala ya Mungu. Biblia inasema katikati yetu sisi na Mungu kuna kile ambacho biblia inakiita hati ya mashtaka "(Kolosai 2:14) kiweke kitabu katika kiganja cha mkono wako wa kushoto kinachotazama juu na kiache kitabu hicho hapo wakati ukiendelea na maelezo Hivyo dhambi zetu hututenga sisi na Mungu.

Hakika, maandiko husema Mungu ni msafi mno kiasi kwamba hata kama ngeandikwa mstari mmoja tu katika kitabu hiki huo tu ungetossha kukutenga wewe na upendo wa Mungu.

Lakini dhambi ni zaidi ya kusema au kufanya kitu Fulani kibaya. Ni mwenendo wa nasi uliomo ndani yetu dhidi ya Mungu tunapoamua kutomsikiliza na kuendesha maisha yetu kama tupendavyo. Hii ndio maana ya DHAMBI kibiblia. Ule mwenendo wa uasi ndio uasi msukumo mkubwa unaotuongoza kutenda dhambi nyingi.

Hebu niweke kiza zaidi katika picha. Biblia inasema, ingawaje Mungu ni upendo, yeye pia ni mwenye haki. Mungu huchukia uovu wote na lazima aiadhibu dhambi. Nabii mmoja katika biblia kumwelezea Mungu namna hii:-

"macho yako ni matakatifu mno, hayawezi kuangalia uovu, na hayawezi kuvumial kuona watu wakitenda mabaya"
(Habakuki 1:13)

Hivyo tuna matatizo mawili kwanza, sisi sote tutaona maovu mengi yaliyo andikwa katika vitabu vyetu binafsi binafsi. Pili, ni lazima maovu yetu yaadhibiwe na Mungu.

Sasa, nielezee kilichotokea wakati ule Yesu alipotundikwa msalabani.

Kwa mfano mkono huu ukisimama badala ya Yesu. Nyoosha mkono wako wa kulia huku kiganja kikitazama juu na huku mkono wako wa kushoto ukiwa unashikilia kile kitabu dari likiendelea kusimama badala ya Mungu.

Hakuna kitabu kati ya Yesu na Mungu yeyesikuzote alimtii Mungu. Siku zote aliyafanya mapenzi ya Mungu.

Sasa Yesu alipokuwa msalabani, Mungu alizichukuwa dhambi za watu wote vizazi vyote akaziweke juu yake msalabani.

"Sasa hamisha kitabu kutoka mkono wako wa kushoto kwenda mkono wa kulia"

12

Petro huielezea namna hii:- "kristo mwenyewe alibeba dhambi zetu mwilini mwake msalabani" (1 Petro 2:24) na Paulo anasema, "Kristo hakuwa na dhambi lakini kwa ajili yetu Mungu alimfanya aishiriki dhambi yetu……."
(2Korintho 5:21)

Waweza kusema kuwa pale msalabani Yesu alifanyika mwenye dhambi kuliko watu wote ambao dunia imewahi kuwa nao, kwani dhambi za mamilioni na mamilioni ya waamini wa vizazi vyote ziliwekwa juu yake.
Lakini kitu cha ajabu kikatokea. Kumbuka, Mungu lazima aadhibu uovu wote!
Hivyo Mungu akaimimina ghadhabu ambayo ilikupasa wewe na mimi. Waweza kusema Mungu alimsulubisha mwanawe mwenyewe.
Ili kuonyesha kuwa tayari alishughulikia tatizo la dhambi zetu ana hukumu baada ya siku tatu Mungu alimfufua Yesu.
Warudishe watu sasa katika mkono wa kushoto ambao hamna kitu, kiganja kikiwa bado kinaelekea juu Sasa yabidi tuulize je ni dhambi kiasi gani zimesalia kwa wale wanao mwamini Yesu mbele za Mungu? Wekea mk azo hapo mpaka mtu Fulani aseme “hakuna”
Hivyo basi mtu akimwamini Yesu Mungu humhesabia mtu huyo kuwa hana dhambi na mkamilifu mbele zake, kwa hakika makamilifu kama Yesu Kristo mwenyewe. Endelea kusisitiza kwamba huu msamaha hautokei kwa kila mtu tu moja kwa moja bali ni kwa wale wanaoipokea neema ya Mungu kwa kumpokea mtoaji wa neema hiyo Yesu Kristo.

Malipo ya kutukomboa

Maelezo yafuatayo yatasaidia kuelezea kifo cha yesu kwa ajili ya kulipia ukombozi wetu. Kama kile kitabu yanaweza pia yakatumika katika somo la pili swala ni kwamba malipo haya yalikuwa ni ya thamani ya juu mno kwa ajili ya kurudisha kile kilichopotea au kuibiwa na kutumikishwa utumwani.
Tumia mmoja wapo ya mifano hii ili kuelezea dhana ya “malipo ya kutukomboa”
1. Katika nyakati za dola ya Kirumi askari waliotekwa waliweza kukombolewa kwa kulipiwa kiasi cha bei au thamani iliyodaiwa na adui.
2. Watumwa wakati wa dola ya Kirumi wangeweza kujikomboa wenyewe. Kama mtumwa angeweza kuweka akiba ya fedha basi angeweza kuupata uhuru wake kwa kujilipia mwenyewe.
3. Maduka ya rehani yamejulikana vizazi vyote. Mtu anaweza kukomboa mali au vitu vyake alivyoviweka rehani kwa kutoa kiwango anachodaiwa.

Dhumuni

Dhumuni la somo hili ni kukamilisha utafiti huu mfupi wa huduma na kufufuka kwa Yesu, na kueleza mambo matatu ambayo mtu lazima anaamini kama anataka kuwa mkristo.
- Hali yake ya kiungu
- Kifo chake kwa ajili ya ondoleo
- Kufufuka kwake

SOMO LA TATU

1. Kazi ya nyumbani

Kundi liliagizwa kusoma Marko sura 6-10. uliza kama yuko mwenye swali kuhusiana na fungu walilosoma au imani ya ukristo. Ruhusu muda kiasi kwa hili.

2. Marudio ya somo la kwanza na la pili

Toa alama dakika mbili hivi za marudio ya somo la kwanza na la pili ili kuamsha kumbukumbu zao.

3. Kutabiriwa kwa ufufuo

Anza kwa kuwaambia kuwa katika maeneo mengi Yesu alitamka kuhusu kufa na kufufuka kwake soma Marko 10:32-34

4. Ufufuo kweli

Soma maelezo ya Marko kuhusu ufufuo – sura 16:1 – 8, ni fupi kuliko injili nyingine. Eleza kuwa zilikuwepo angalau nyakati kumi tofauti ambazo Yesu aliwatokea wanafunzi wake.

5. Ufufuo maana yake halisi

Uliza: Ulishawahi kufikiri ulipokuwa motto dunia ingekuwaje bila wewe? (mfano, kama ungekufa) toa maoni hapa kuwa, swala la kifo na maisha baada ya kifo limesumbua wengi katika vizazi vyote. Baada ya kifo kunatokea nini? Je kuna mbinguni, jehanam au hakuna chochote? Mwandishi mmoja aliandika hivi:-
“Kifo chenyewe si kitu

lakini hili twaliogopa kuwa hatujui kipi, hatujui wapi”
Katika biblia majibu ya maswali haya yanapatikana katika ufufuo wa Yesu soma Matendo 10:39-43
Eleza kuwa Petro alikuwa akizungumza na Kornelio, mtu asiye mjua Kristo. Ona anachosema Petro. Haya ndiyo aliyoamuru Yesu yafundishwe (mstari 42) kuna mambo matano ya kuona katika habari hii. Chapa maelezo haya katika kadi na fundisha kwa kutoa kadi moja moja.
(a) Watu wote watafufuliwa (mstari 42)
Ina maana “walio hai na wafu”
Biblia yaizungumzia siku ambayo walio hai na wafu wa vizazi vyote watafufuliwa.
(b) Watu wote watahukumiwa
Yesu atawahukumu walio hai na wafu (mstari 42) sisi hatuko huru kujiamulia lazima tutatoa hesabu ya matendo yetu kwa Mungu aliyetupa uhai.
(c) Jesu aliyefufuka atakuwa hakimu siku ile
Yesu ndiye aliyechaguliwa na Mungu kuwa hakimu siku ile (mstari 42)
Ndio maana ufufuo wa Yesu ni wa muhimu sana. Si kwamba unatuhakikishia ufufuo wetu sisi tu bali anatuhakikishia hukumu yetu. Tunawajibika kwa Yesu.
(d) Watu wote wagawanywe makundi mawili
• **kundi la kuume**

SOMO LA TATU

YESU – KUFUFUKA KWAKE

14
Wale waliomwamini Yesu – sasa waliosamehewa – sasa watapokelewa na Yesu siku ya hukumu (mbinguni)
• **kundi la kushoto**
Soma Marko 8:38
Wale wanaomkataa Yesu – sasa watakataliwa na Yesu – siku ya hukumu (jehanamu)
Mifano mingi ya Yesu huzungumzia mgawanyo huu. Alizungumza mfano wa magugu na ngano, kondoo na mbuzi, samaki wazuri na wabaya.
(e) Mgawanyo huu ni wa milele
Katika biblia hakuna dhana ya kupata nafasi baada ya kifo maisha yetu ya sasa ndio nafasi na ya pekee.
Hitimisha kwa kusema
Mwenendo wako kwa Yesu leo ni sawa na mwenendo wa Yesu hapo mbeleni.
Ukimkubali leo, atakukubali hapo aadaye.
Ukimkataa sasa, atakukataa hapo baadaye (ona pia 2 thesalonike 1:9-10)

6. Ufafanuzi kwa stuli ya miguu mitatu

Elezea kwamba tumeshaona sasa dhana kuu tatu za msingi ambazo ndizo kiini cha ukristo

7. Kazi ya nyumbani

Liagize kundi kusoma Marko 11-16, wakumbuke kunakili vifungu wasivyoelewa au vile ambavyo wangependa kujadili muda utatolewa kujadili wakati wa somo lijalo mwanzoni toa kitini(*hand out)*namba 3

15

Dhumuni

Dhumuni la somo hili ni kufundisha dhana iliyo ngumu (ni ngumu kwa sababu ni ngeni kabisa kwa wanadamu wanaojivuna na wenye asili ya dhambi) ya kwamba tunaokolewa kwa neema ndani ya kristo Yesu, na wala si kwa juhudi zetu au matendo yetu

SOMO LA NNE

1. Kuipitia kazi ya nyumbani

Washiriki waliagizwa kusoma injili ya Marko sura 11-16 waulize endapo wana maswali kutoka katika sura walizosoma au katika eneo. Katika imani ya kikristo ruhusu muda kwa ajili ya jambo hili.

2. Marudio ya masomo matatu yaliyopita

Mtu hawezi kamwe kuwa mkristo kwa maana halisi ya neno hilo kibiblia bila kuamini misingi hii mitatu ya imani ya kikristo
- Yesu –uwana wake(asili yakeya kiungu)

- Yesu – msalaba wake (kufa kwake badala yetu)
- Yesu – ufufuo wake (ubwana wake)

3. Utangulizi wa somo

Wape washiriki karatasi na kalamu na watake waandike majibu ya maswali mawili mawili.

Waeleze kuwa hakuna mtu atakayeona majibu yao. Anza kwa kuuliza swali hili. "Je unao uhakika kwamba wewe utaurithi uzima w milele" - hii ina maana kuwa kama ungekufa sasa hivi utakwenda mbinguni?

Wengi waweza wakajibu, "Hapana" au "sina hakika" Hivyo waambie dakika chache zijazo nitakuelewesha jinsi utakavyokuwa na uhakika wa jambo hili. Kabla sijakuelewesha nikuulize tena swali jingine ambalo litasaidia kufafanua zaidi swala hili. Halafu uliza: "kama ungekufa leo na ukasimama mbele ya Mungu wa mbinguni na akakuuliza, "kwa nini nikuruhusu kuingia mbinguni?" utamjibuje?

Watakapokuwa wamejibu, maswali yote toa bahasa mbili kubwa (nashauri saizi 305 x 155 mm bahasha ngumu)

Bahasha namba 1- ina x kubwa nyuma yake na maneno haya WOKOVU KWA MATENDO, ndani ya bahasha hii kuna bahasha ndogo (nashauri saizi 235 x 120 mm
bahasha ya karatasi ngumu) Bahasha hii ina
maneno "YALE NILIYOTENDA MIMI" mbele Neno mimi likaziwe ndani ya bahasha
hii kuna kadi zenye maneno haya tofauti tofauti katika kila kadi

- matendo yangu mema; kutimiza amri kumi; kutotukana, kutosema uongo, kutoiba; kutoa misaada raia mwema; kutunza familia; kusoma biblia na maombi; kwenda kanisani ubatizo; kipaimara; usharika mtakatifu.

Bahasha ya 2 ina kijiti kikubwa nyuma na maneno wokovu KWA IMANI mbele yake.

Ndani ya bahasha hii mna bahasha ndogo kama kwangu iliyoandikwa ALIYOTENDA
KRISTO yamechapwa mbele ya bahasha. Neno KRISTO likiwa limekaziwa. Ndani ya
bahasha hii kuna ule mchoro wa stuli ambao
tuliuona katika somo la 1,2 na 3 (tazama mchoro ukurasa 52)

Waeleze kuwa yapo majibu mawili kimsingi,
kwa yale maswali yaliyoulizwa moja ni sahihi
na jingine si sahihi.

4. Jibu lisilo sahihi niliyotenda mimi

Tutalitazama jawabu lisilo sahihi kwanza waonyeshe bahasha yenye msalaba nyuma. Kisha waonyeshe maneno ya mbele ukielewesha kuwa WOKOVU KWA

SOMO LA NNE

NEEMA – SI MATENDO YETU

16

MATENDO hukazia YALE NILIYOTENDA
MIMI. Fungua bahasha hii kisha toa kadi zilizo ndani moja moja.

Waeleze kuwa hivi ndivyo watu wanavyojaribu kujipatanisha na Mungu lakini
hakuna tendo moja au matendo yote hayo kwa
pamoja yangeweza kutupa kibali mbele za Mungu

Waulize swali hili "Kwa nini" matendo mema hayawezi kutupa kibali cha kuingia Mbinguni?

Soma *Marko 7:20 – 23*

Waeleze kuwa viwango vya Mungu ni ukamilifu asilimia 100 – na kwa viwango hivi
sote hatustahili. Hii ndio maana hakuna atakayeokoka kwa matendo mema.

Pili, dhambi si tu lile unalolifanya, au unalosema au lile baya unalolifikiri. Yesu

anasema hapa kuwa toka ndani, kutoka katika
mioyo, hutoka maovu yote aliyo yaorodhesha.
Kwa mfano ukimwendea daktari ukiwa na madoadoa usoni naye akasema una tetemaji.
Na akijaribu kukutibu kwa kuweka dawa kwenye majeraha tu utamwambia Daktari hapana kwani yale majeraha huonyesha tu kuwa upo ugonjwa bali ugonjwa halisi si huo bali upo katika mkondo wa damu. Ndivyo ilivyo pia kwa dhambi.
Tunaposema hilo ni baya linadhihirisha tu kile kilichopo ndani ya mtu. Shida halisi iko ndani. Biblia inasema ndani ya mioyo yetu tumemwasi Mungu kwa kujua au kutokujua na kule kutenda matendo mema hakutotusaidia kuondoa uasi ulioko ndani yetu. Kufanya matendo mema ni sawa tu na kufunga yale majeraha yaliyo juu.
Tatizo kubwa tulilo nalo ni kwamba twataka kuendesha maisha yetu wenyewe tupendavyo.
Twataka tuwe mbali na Mungu. Hii ni dhambi.

5. Jibu sahihi yale aliyotenda kristo.

Onyesha alama ya tiki nyuma ya bahasha, halafu mbele maneno WOKOVU KWA NEEMA.
Uliza: “Kwa neema ina maana gani? Waeleze kuwa hii ina maana zawadi tusiyostahili. Toa bahasha ndogo yenye maneno “YALE ALIYOTENDA KRISTO”
Fungua bahasha ndogo kuonyesha mchoro wa stuli onyesha kile alichotenda Kristo kwa niaba yetu..
Soma *Waefeso 2: 8 – 10.*
Waeleze kuwa ni neema kwa Imani pekee tutaokoka. Wokovu huu ni kipawa cha Mungu.
Tandaza bahasha zote ndogo oanisha maneno haya “YALE NILIYOTENDA” na “YALE
ALIYOTENDA KRISTO” Fafanua kuwa ni kazi ya Kristo iliyomalizika tayari ndiyo ituokoayo. Lazima tuikubali kazi yake iliyokamilika kwa imani.
Kufikia hatua hii utapata mwitikio wa namna hii, “Ikiwa wokovu ni zawadi ya bure basi hii si yamaanisha kuwa naweza kuishi maisha yoyote nitakayo na ili mradi naamini Mungu si atanisamehe? Hii si yamaanisha matendo si muhimu?
Fafanua kutoka Waefeso 2:10 ya kuwa Mungu anatutaka tuishi maisha yenye matendo mema, lakini haya lazima yawe ni matokeo ya wokovu.
Mchoro huu waweza kusaidia.
Zingatia ya kwamba matendo mema hayampi mtu wokovu (Waefeso 2:8 – 9) lakini wokovu

MATENDO MEMA WOKOVU

WOKOVU **MATENDO MEMA**

humfanya mtu kuishi maisha yenye matendo mema (*Waefeso 2:10*).
Angalia *Marko 10:15* mahali ambapo Yesu alitilia mkazo kwamba ufalme wa Mungu lazima upokelewe kama mtoto mdogo.

6. Tamati

Wakumbushe kuwa uliwaambia kwamba utawaonesha jinsi ya kuwa na hakika ya uzima wa milele. Tumeona kuwa hatuwezi kuupata wokovu kwa matendo yetu mema. Ni karama ya Mungu.
Hitimisha kwa kusema kuwa zawadi lazima ipokelewe. Vivyo hivyo neema ya Mungu pia.
Wiki ijayo tutaona namna tunavyoweza kupokea Karama (zawadi) hii ya uzima wa milele.

7. Kazi ya nyumbani

Mpe kila mmoja kipeperushi cha Uinjilist –
kutoka katika kitabu hiki au chochote kile unachokifahamu. Hakikisha mwisho wa kipeperushi kicho kuna sala ya toba yenye kukazia ubwana wa Yesu. Waagize kukisoma kipeperushi kwa makini. Wawekee alama maeneo wasiyoelewa au yale watakayo kuja jadili.

Pia waagize kusoma vifungu hivi vya Marko na wapigie mistari maneno yenye uzito au mkazo.
Marko 1:15 Marko 8:34 – 38
Marko 9:43 – 48 Marko 10:29 – 31
Wape kitini namba 4
18
19

Dhumuni

Dhumuni la somo hili ni kujibu swali: Mkristo ni nani? Anza kwa kufanya marudio ya haraka ya somo la 1 – 4

Marudio ya kazi ya nyumbani

Wanakikundi waliagizwa kusoma kipeperushi na sura kadhaa za injili ya Marko, uliza kama wana maswali na ni maneno gani ya msingi ambayo wameyapigia mstari. Ni kwanini maneno hayo yamekuwa na mkazo au uzito kwao?

SOMO LA TANO

1. Ufunguzi

Kwa mfano tukiamua kufanya utafiti madukani. Tunalo swali moja tu: "Kwa mtazamo wako wewe Mkristo ni nani? Utapata jibu la namna gani?
Wana kikundi wanaweza kujibu namna hii.
Mtu mwema anayekwenda Kanisani ……
mwenye kutimiza amri kuu ……..
anayeishi katika nchi ya Kikristo …….
Na kadhalika.
Waeleze kuwa katika hatua hii utazungumzia kuhusu Mkristo ni nani.

2. Mstari mkuu: *Marko 1: 15*

Kwa sentensi moja, Mkristo ni mtu ambaye yumo ndani ya ufalme wa Mungu. Hii humaanisha ni pale Yesu anapofanyika mfalme au Bwana wa Maisha yako.
Katika *Marko 1:15* Yesu anasema yapo mambo mawili, mtu anaweza kufanya ili aweze kuupata ufalme wa Mungu.
Ni Yapi?
• TUBU
(Geuka na kuziacha dhambi zako).
• AMINI
Leo tunaangalia toba.

3. Toba ni nini?

Unakuwa Mkristo unapomfanya Yesu Mfalme na Bwana wa maisha yako.Kwa maneno mengine.
(Onyesha maneno haya kwenye kadi)
Soma: *Marko 8:34 – 38*
Uliza: Je toba ina maana gani hasa?
Inamaanisha namweka Yesu mbele katika mambo haya:-
(Ongeza kadi hii)
Yesu anasema mtu lazima asahau (au ajikane)
nafsi, na kuubeba Msalaba wake na kuipoteza nafsi yake. Hivyo msalaba ulikuwa chombo cha mauti. Yesu ananiambia mimi, ikiwa nataka kumfuata, lazima nipitie namna ya kifo (mauti).
Lazima nife kutoka katika haki ya kuendesha maisha yangu (ambayo ni dhambi).
Lazima nijiweke chini ya haki ya Bwana Yesu aliyopewa kuwa mfalme wangu.
Tumia kielelezo cha nyumba katika ukurasa wa ?? ili kusaidia kufafanua maana ya hili. (Ongeza kadi hii.)
Lenga *Marko 8:36 – 37*

Namtanguliza Yesu

… Kabla ya mapenzi yangu

SOMO LA TANO

MKRISTO NI NANI

1. Kutubu

20
Watu kila mahali wanajaribu kuipata dunia yote. Kwa kiwango kikubwa au kidogo lengo lao ni kututa mali, kuwa na nguvu, umaarufu, kujulikana na mafanikio katika biashara au tu kuwa mbele ya majirani zake.
Mambo haya yaweza yasiwe mabaya kimsingi lakini yatakuwa ni dhambi kama twaishi kwa ajili ya hayo juu ya vitu vyote.
Tunapompa Yesu nafasi yake ya kwanza vitu hivi vitakaa katika nafsi yake.
Waweza kunukuu maneno ya Yesu.
"Tafuteni kwanza ufalme wa Mungu na hayo mengine mtazidishiwa"
(Mat. 6:33)

(Ongeza kadi hii.)
Lenga *Marko 8:38.*
Si jambo la kawaida kumfuata Yesu kwa uaminifu leo marafiki na ndugu waweza kuniona mimi ni mtu wa ajabu... wengine hawatapenda kujihusisha na mimi tena. Lakini kama nitamwonea Yesu aibu katika maisha haya yeye naye atanikataa siku ya hukumu lazima nimfuate Yesu wazi wazi. Hapendezwi na wanafunzi wa siri.
Jambo ambao ni lawazi zaidi la kumkubali Yesu wazi wazi ni kujiunga na Kanisa. Watu hukwepa kujiunga na Kanisa kwa kusema kuna udhia, lakini kiukweli wao hukwepa kujihusisha na Yesu pamoja na watu wake wazi wazi.
Sisitiza ya kuwa unaweza kuwa na mwenzi wa ndoa, ndugu au rafiki ambaye hakubaliani na imani yako. Lakini endelea kumtanguliza Yesu hata kama utadhihakiwa. (Hapa hatumaanishi umwache mwenzi wako).
(Ongeza kadi hii).
Soma *Marko 9:43 – 48*
Yesu hapa hamaanishi mivikate viungo vyangu vya mwili. Anamaanisha kama kitu au mtu ananizuia kuingia katika ufalme wa Mungu hapo pahitajika upasuaji halisi. Weka wazi kwamba kiburi ndicho hasa kinachozuia watu.
• Kwa kiburi changu sikubali kuupokea wokovu kama zawadi.
• Kwa kiburi changu siko tayari kujitiisha kwa Yesu kama mfalme.

4. Ni Ngumu?

Mwisho soma, *Marko 10:29 – 31*
Yawezekana ikiwa ni vigumu kumfuata Yesu lakini anatuahidi mambo mawili tunapomfuata.
(1) Katika maisha haya atatulipa mara mia, kwa gharama yoyote tutakayoitoa.
(2) Katika maisha yajayo atatupa uzima wa milele.

5. Hitimisho

Lionyeshe kundi ile sala ya toba ndani ya kijitabu. Washauri waitumie hiyo sala, kibinafsi nyumbani wakimaanisha kabisa kwamba wanatubu mbele za Mungu. Tutaitazama tena hiyo sala wiki ijayo.
Malizia kwa marudio kwa ufupi.

…. Kabla ya jitihada zangu za mafanikio
…. Kabla ya umaarufu Wangu
…….. Kabla ya……?

6. Kazi ya nyumbani

Warudie kusoma kipeperushi ulichowapa. Kutoka katika kitini anao wajibu maswali kutoka Marko.
Ni zawadi gani anayotoa Mungu kwa wale wanaoamini na kutubu?
Marko 1:8
W_ _ _ _ _ W_ _ _
Marko 2:10
M _ _ _ _ _ _ wa D _ _ _ _ _
Marko 10:30
U _ _ _ _ wa M _ _ _ _ _ _
Gawanya kitini cha somo la 5.
Roho Mtakatifu hataridhika kukaa sebuleni tu. Mara tu atakapoingia maishani mwangu, atataka kunibadilisha niwe katika sura yake.
Hili halifanyiki mara moja – hii ni kazi ya muda mrefu hatua kwa hatua.

Nyumba

Kieleleze kitakacho saidia kuonyesha kuja kwa Roho Mtakatifu ndani yetu kwa matumizi ya somo la 5.
Kwa ufafanuzi, ninapo mpokea Yesu yeye huja na kukaa na mimi kiroho kwa Roho wake mtakatifu. Ni hivyo basi kadiri siku na miaka iendavyo Roho Mtakatifu hutaka kunibadilisha mimi kabisa niwe kama Yesu.
Utahitaji mchoro wa ramani ya nyumba kama hii hapa.
Eleza kwamba unaponunua nyumba kuna hatua mbili za kufuata.
• ***Siku ya kuingia*** (Hii hutokea mara moja tu).
• ***Ukarabati na upambaji***
(Hii huendelea kwa muda mrefu kadri unavyokaa kwenye hiyo nyumba.
Vivyo hivyo kwa maisha ya Mkristo zipo hatua mbili.

1. Kuongoka na Kufanywa Mkristo

Hili hutokea Mungu anapompa neema ya

kutubu na kujiachia mikononi mwa Yesu – anaponifungulia mlango na kwa njia ya Roho Mtakatifu huja kuishi nami. Hili hutokea kwa uhalisi mara moja, ingawaje kuna Wakristo wengi ambao hawawezi kusema kwa hakika ni siku ipi iliwatokea hivyo.
Hapa tunasema umezaliwa upya, na

G e u k a
T e g e m e a
S a f i r i

mwamini.

2. Kuwa Mkristo

Wajulishe kuwa vyumba mbalimbali katika hiyo nyumba husimama badala ya maeneo mbali mbali ya maisha yangu: NDOA, FAMILIA; MALI; JUHUDI; STAREHE; NGONO; WAKATI N.K. Roho mtakatifu haridhiki kukaa sebuleni tu >
Aingiapo maishani mwangu,atataka kunibadilisha kwa sura yake. Hili halitokei mara moja bali hutokea taratibu hatua kwa hatua, kama kule kukarabati nyumba. Tunasema haya ndiyo maisha mapya au utakaso unaoendelea. Hili liko wazi. Ninapokuwa Mkristo lazima niwe radhi kumfanya Yesu Bwana wa yote. Uhiari huu ndio mwanzo wa toba. Roho wa Mungu atakuwa akitenda kazi ndani ili kulitekeleza hilo kadri ninavyokuwa katika maisha haya mapya.

Dhumuni

Dhumuni la somo hili ni kuendeleza somo la 5 na kujibu swali.
Nawezaje kuwa Mkristo?
Mwishoni mwa somo hili washiriki wataombwa kujaza fomu ya tathimini ya kozi hii

SOMO LA SITA

1. Kupitia kazi ya nyumbani

Washiriki waliagizwa kusoma sura tatu katika Injili ya Marko. Je wamegundua nini kuhusu vipawa atoavyo Mungu kwa wale wamjuao Yesu? Jadili.

2. Utangulizi

Wiki iliyopita katika kupitia swali:- Mkristo ni nani? Tuliona.

• kristo ni mtu ambaye yumo ndani ya ufalme wa Mungu (Marko 1:15), hii humaanisha anaye Yesu kama mfalme.
• Ili niweze kuwa ndani ya ufalme huu lazima NITUBU (Somo lililopita).
• Ili niweze kuwa ndani ya ufalme huu lazima NIAMINI (Somo la leo).

3. Imani au kuamini nini?

Tunaangalia matukio matatu katika Injili ya Marko ambayo hufafanua Imani.
Soma *Marko 5:21 – 24, 5:35 – 43*
Onyesha kadi hizi.
Yairo alijisikiaje alipojulishwa kifo cha binti yake. Imani hapa ni kusimama katika neno la Yesu bila kujali mazingira yoyote yaliyo kinyume. Haitegemei jinsi tunavyojisikia bali hutegemea yale aliyosema Yesu. Usiogope, amani tu (Mst. 36).
Tumia kielelezo katika ukurasa IMANI/ HISIA/ KWELI.
Soma *Marko 5:25 – 34 ongeza kadi hii*
Soma *Marko 10:13 – 16 ongeza kadi hii*
Hapa sio ile imani kama ya mtoto anayozungumzia Yesu. Hapa ni zaidi ya kupokea kiufahamu. Inamaanisha tegemeo kama lile la mtoto kwa wazazi wake.
Tumia kielelezo cha BLONDINI katika ukurasa Soma *Yohana 5:24.*Ongeza Kadi hii. Hili humjulisha mwamini kitu kuhusu sasa na pia kuhusu wakati ujao.

IMANI NI…….

…KUMWAMINI YESU SAWA NA NENO LAKE
….KUMWENDEA YESU KUJUA MUNGU NANIKUBALI

SOMO LASITA

MKRISTO NI NANI

2. Kuamini

INAMAANISHA TEGEMEO KAMA LILE LA MTOTO KWA WAZAZI WAKE

(a) Sasa “ana …….Uzima wa milele sisitiza wakati ulipo, ‘ana’.
Unaposema “Najua ninao uzima wa milele”, si kwamba unajigamba. Utakuwa ukiamini kile Mungu alicho sema, hiyo ndiyo Imani. Hivyo si kusema “mimi ni mwema” ila kusema kuwa alichofanya Yesu, ndicho kinanifanya nikubaliwe na Mungu na sio nilichofanya mimi.
(b) Wakati ujao: “hatahukumiwa”
Hapa, Yesu anazungumzia hukumu ya milele Mbinguni au Jehanam mwamini hata hukumiwa, maana hakuna shitaka litakaloletwa dhidi yake.
Ongeza kadi hii.
Kumbuka maneno ya Yesu.
Yeyote asiyeupokea ufalme wa Mungu kama mtoto hatauingia kamwe.*(Marko 10:15).*
Tumeona kuwa kuupokea ufalme wa Mungu mtu lazima ampokee Yesu kama Bwana au mfalme na mwokozi wa dhambi zake. Hii ni hatua ya kibinafsi. Hakuna awezaye kuchukua hatua hii kwa niaba yako.

4. Hitimisho

Kufikia hatua hii hitimisha kozi kwa njia moja au mbili.
Wakristo wengi hupata shida katika kuwaongoza wengine kumpokea Yesu. Kama

Njia ya kuvuta kwa taratibu

Waweza kusema hivi:- Yawezekana Mungu amesema na wewe katika kozi hii. wewe ni mmoja wa hao fuata utaratibu huu.

• Pengine uko tayari sasa kuchukua hatua ya kumpokea Yes awe Bwana na mwokozi wako. Napenda kukusaidia kuchukua hatua hiyo.
• Waombe wafungue mahali penye sala ya toba katika kile kipeperushi.
• Wasomee ile sala ya toba.
• Washauri waombe sala hii wenyewe mbele za Mungu wawapo nyumbani kama ishara ya kumkubali.
• Watake wakujulishe watakapokuwa wamechukua hiyo hatua ili uweze kuwapa msaada watakao uhifazi baadaye.

Njia ya moja kwa moja

Kama unao uhakika kuwa wako tayari kutoa maisha yao kwa Yesu basi hitimisha namna hii:-

• Yawezekana Mungu amezungumza na wewe kiroho kupitia kozi hii na huenda sasa uko tayari kumpokea Yesu awe Bwana na mwokozi wako.
• Waagize kufungua mahali sala ya toba ilipo katika kile kipeperushi ulichowapa.
• Soma sala ile kwa sauti, kisha sema: Nitakwenda kusali sala hii tena taratibu, kama uko tayari kuchukua hatua basi na kushauri uombe sala hii pamoja na mimi.
• Rudia kuomba sala ile kwa sauti taratibu.

Neno la tahadhari

Roho mtakatifu ni mkuu na hutawala yote katika uinjilisti. Ni yeye tu awezaye kugeuza moyo wa mtu na fahamu zake kikweli.
Haimpatii Mungu heshima tunapowashawishi watu kwa hila ili wafanye uamuzi endapo hawako tayari kufanya hivyo.
Ikiwa hatuna hakika na msimamo wa mtu katika kufanya uamuzi ndani ya kundi basi tutumie ile njia ya kwanza.

5. Tathimini ya kozi

Mpe kila mtu nakala ya Fomu ya Tathimini ya kozi na kalamu (angalia ukurasa wa 44)

…… KUMPOKEA YESU KAMA MFALME WAKO

25

Waeleze kwamba hawalazimishwa kujibu maswali.Kusanya fomu hizo mwishoni.
Fuatilia kozi ya uanafunzi.
Weka msisitizo katika swali la 6 unapopitia ile fomu ya Tathimini ya kozi.
Kama wamekubali kujiunga na kozi, basi fanya utaratibu wa kuanza hiyo pamoja nao.

26

HABARI ZA BLONDIN

Kielelezo kitakachofaa kuelezea imani kwa matumizi ya somo la sita.
Dhumuni ni kuonyesha kuwa inawezekana kuiamini Injili kiakili na kinadharia bila kujitoa kikamilifu kwa Yesu

Blondini alikuwa mtu maarufu huko marekani aliyeweza kutembea juu ya iliyokazwa na kufanya michezo mbambali ya hatari.
Miaka kadhaa iliyopita alifunga kamba juu ya mapopromoko ya mto Niagara na akatembea juu ya kamba hiyo.
Siku moja alitangaza kwamba atavusha mtu akimwendesha ndani ya mkokoteni juu ya kamba ile ngumu.
Amwndishi wa habari alikuja kumhoji Blondini kuhusiana na tangazo lake hilo.Blondini alimwuliza “Je unaamini kuwa ninaweza kufanya hili ?”.
“Hakika naamini kuwa unaweza,” mwandishi alijibu. “Nafikiri wewe ni hodari katika mchezo huu kuliko wote duniani”
“Waamini naweza kufanya ? “, Blondini aliuliza tena, “ Basi sasa ingia katika mkokoteni nikuvushe ! “
Kuna tofauti kati ya kumwamini mtu kinadharia na kuwa tayari kujikabidhi kwake kikamilifu kwa imani.

Kweli, Imani na Hisia

Vielelezo vya kusaidia kufafanua maana ya imani vitakavyo tumika katika somo la sita.
Dhumuni la kilelezo hiki ni kuonyesha kuwa imani ya kikristo haitegemi hisia zetu ambazo hubadilika mara kwa mara, bali hutegemea ukweli wa kile alichofanya Mungu kupitia Yesu kama ilivyoandikwa katika biblia. Kweli hizi haizibadili kamwe. Waweza kutoa kielelezo hiki kwa maneno lakini mchoro kama huu waweza kusaidia.
Watu watatu wanatembea juu ya ukuta mwembamba. Mtu wa kwanza anaitwa ‘KWELI’ wapili “IMANI na watu ‘HISIA’ Wakati wote mtu huyu wa katikati Imani” anapomtazama “Kweli” atatembea kwa usalama na amani juu ya ule ukuta. Akigeuka na kuangalia nyuma yake kwa ‘Hisia’ ataanza kuyumba na kuogopa. Vivyo hivyo katika maisha ya Kikristo, Imani, thabiti imesimama katika kweli kuhusu Yesu kama

Maana ya Ukristo tathmini ya kozi

Weka tiki majibu sahihi
Tafadhali uwe wazi na mkweli
Usilazimike kujibu usilotaka kujibu
Jina…….
……..Simu…….
1. Kabla ya kuanza kozi hii ungetaka kusema nini kuhusu wewe mwenyewe?
a. Sikuwa naamini kuhusu Mungu.
b. Skuwa hakika kuwepo kwa Mungu au la
c. Nilimwamini Mungu na sio Yesu Kristo
d. Nilifikiri nilikuwa mkristo , lakini sasa najua sikuwa
e. Mimi ni mkristo (yaani ,aliyejitoa kwa Yesu Kristo)
f. Kitu kingine…….
……..
2. Waielezeaje sasa nafasi yako ya uhusiano na Yesu Kristo
a. Nimetubu kwa kumaanisha na kumwamini Yesu Kristo na nimempokea kama Bwana na mwokozi wangu
b. Natamani kujifunza zaidi , lakini kwa sasa bado sijatoa maisha yangu kwa Yesu .
c. Mengineyo……..
……..
3. Kama bado hujawa mkrosto ni nini kinachokuzuia ?
.....
.....
.....
.....
.....
4. Katika mwendo wako wa maisha ya kiroho je umeshafikia mahali pa kuwa na uhakika wa uzima wa milele ? Ukifa leo utakwenda mbinguni ?
 NDIO HAPANA
5. Mfano ungekufa leo na ukasimama mbele ya Mungu na akakuuliza, “Kwa nini nikuruhusu kuingia mbinguni ? Utajibuje ? “Uniruhusu kwa sababu
……
……
……

……
……
……
……
……
……
……
6. Mara nyingi watu wanaomaliza kozi hii hupenda kujifunza zaidi mambo yahusuyo imani ya kikristo kuhusinan na hitaji hilo twatoa kozi ya wiki sita inayohusu maana ya kuwa mwanafunzi , mfuasi wa Yesu Kristo, Je ungependa kujiunga na kozi hiyo NDIO HAPANA BAADAYE
7. a. Natoshelezwa na kanisa niendalo.
b Siendi kanisani , lakininiependa nitambulishwe kwa kanisa ambalo lina ushirika
mzuri na mafundisho mazuri.
c. Sihitaji kwenda kanisani kwa sasa
8. Una maoni gain kuhusu kozi hii ? (yawe mazuri au mabaya)
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……..

UFUPISHO WA KILA SOMO KWA AJILI YA KUTOA NAKALA

…

Maelezo yafuatayo yamefupishwa kwa kila somo. Ruhusa inatolewa kwa kila kundi kutoa nakala yake. Zimetengenezwa kwa mtindo wa kukunja kama inavyoonesha katika mchoro huu

Maelezo yafuatayo yamefupishwa kwa kila somo. Ruhusa inatolewa kwa kila kundi kutoa nakala yake. Zimetengenezwa kwa mtindo wa kukunja kama inavyoonesha katika mchoro huu